




# WATTS UP AFRICA

## Kuwezesha Mpito wa Afrika ili Kutumia Nishati Jadidifu

Afrika imefikia wakati muhimu. Huku zaidi ya **watu milioni 600 wakikosa huduma ya umeme**, chaguo zinazofanywa leo zitachangia mustakabali wa nishati katika bara hili kwa vizazi vingi. Sisi, mashirika na washirika waliotia saini, tunaungana chini ya kampeni ya **Watts Up Africa** kudai mpito unaozingatia watu na wa haki wa matumizi ya hadi **100% ya nishati jadidifu -** ambao unawezesha jamii, kuendeleza haki ya tabianchi, na kuvunja minyororo ya utegemezi wa mafuta ya visukuku.

Kwa miongo kadhaa, Afrika imechukuliwa kama kitovu cha rasilimali kwa masoko ya kimataifa ya nishati, na kuchochea uchumi mahali pengine wakati watu wake wanabaki katika umaskini wa nishati. Serikali, taasisi za kifedha, na mashirika ya kimataifa yanaendelea kusukuma **nishati ya mafuta ya visukuku, miradi mikubwa ya uchimbaji, na suluhu za uwongo** ambazo hazisaidii jumuiya za Afrika. Badala yake, miradi hii inazidisha **mzozo wa tabianchi, huongeza mzigo wa madeni, na kuendeleza ukosefu wa usawa**.

Tunakataa mtindo huu uliopitwa na wakati. Afrika ina utajiri wa **nishati ya jua, upepo, na jotoardhi**, na mpito wa haki si wa lazima tu - **unawezekana**. Nishati jadidifu inaweza kuimarisha viwanda, kuunda nafasi za kazi, na kutoa umeme wa kuaminika na wa bei nafuu kwa Waafrika wote huku ikihakikisha uendelevu wa mazingira na kulinda haki za jamii.

## Matakwa Yetu

Tunatoa wito kwa serikali za Afrika, mashirika ya kikanda, benki za maendeleo, na washirika wa kimataifa kuchukua hatua za haraka kuhusu yafuatayo:

### 1. Kujitolea kwa Mustakabali wa Nishati Jadidifu na Ukuzaji wa Viwanda Vinavyozingatia Mazingira kwa 100%

- Kuanzisha na kutekeleza **ramani za kitaifa na kikanda za mpito wa nishati** ambazo zinawekea kipaumbele **nishati ya jua, upepo, jotoardhi na mifumo ya nishati jadidifu iliyogatuliwa** ili kuhakikisha **ufikiaji wa nishati kwa wote, kwa bei nafuu na ya kutegemewa** kufikia 2030.
- Kuanzisha **mamlaka ya nishati** kwa kuwekeza katika tasnia ya **nishati jadidifu inayoongozwa na Afrika**, ikijumuisha **utengenezaji wa ndani wa paneli za sola photovolteki (PV, solar photovoltaic), mitambo ya upepo, uhifadhi wa nishati ya betri, na teknolojia ya jotoardhi** ili kuendesha **ukuaji wa viwanda vinavyozingatia mazingira, uundaji wa nafasi za kazi, na ustahimilivu wa kiuchumi**.
- Kusawazisha mikakati ya mpito ya nishati na **Ajenda ya 2063** na **Dhamira ya Madini ya Afrika (AMV)** ili kuhakikisha **uongezaji wa thamani, manufaa ya kindani, na mifumo ya usambazaji wa kikanda** ambayo inazuia utekelezaji wa rasilimali na kuongeza faida za kiuchumi kwa nchi za Afrika.

- Kutambua kisheria **upatikanaji wa nishati kama haki ya msingi ya kibinadamu** na kuanzisha **ahadi za kisera zinazopaswa kufuatwa** na kukomesha utegemezi wa nishati ya visukuku, kuhakikisha **mpito wa haki na unaotoa nishati ya kaboni kwa kiasi kidogo** ambao unawekea kipaumbele mahitaji ya maendeleo ya Afrika.

## 2. Kukataa Upanuzi wa Mafuta ya Visukuku na Suluhu za Uongo

- **Kutekeleza usitishaji wa mara moja** wa utafutaji mpya wa oili, gesi na mkaa, uchimbaji na maendeleo ya miundombinu ambayo yanatishia jumuiya, mifumo ikolojia na uchumi wa Afrika.
- **Kukataa pendekezo la gesi kama fueli ya mpito**, kwa kutambua kwamba gesi **huiweka Afrika katika utegemezi wa nishati ya visukuku**, huweka uchumi kwenye soko tete la kimataifa la nishati, na **kuelekeza uwekezaji muhimu mbali na nishati jadidifu**.
- Kupinga **marekebisho ya kiteknolojia** yanayopotosha kama vile **kunasa na kuhifadhi kaboni kwa kiasi kikubwa (CCS), kulipa wengine kwa upunguzaji wa kaboni, na miradi ya hidrojeni ambayo haina uendelevu na usawa**, ili kuhakikisha kwamba mustakabali wa nishati barani Afrika hauamriwi na masilahi ya kampuni za uchimbaji mogodi.

## 3. Kuhakikisha Upatikanaji wa Nishati Sawa na Jumuishi

- Kuharakisha utoaji wa **suluhu za nishati zisizo kwenye gridi ya taifa, zilizogatuliwa na za gridi ndogo** katika maeneo ya vijijini na maeneo ambayo hayahudumiwi vya kutosha ili kuziba pengo la upatikanaji wa nishati.
- Kutunga **mifumo endelevu ya usimamizi wa nishati** ambayo inahimiza kushiriki kwa **wanawake, vijana, wenyeji, na jamii zilizotengwa** katika upangaji wa nishati, utunzi wa sera, na ugavi wa faida.
- **Kuondoa vikwazo vya udhibiti na kifedha** vinavyozuia matumizi ya nishati jadidifu, ikiwa ni pamoja na **ushuru wa juu, sera zenye vikwazo, na ruzuku za mafuta ya visukuku** ambazo huathiri masoko ya nishati na kukatisha uwekezaji endelevu.
- Kuongeza uwekezaji katika **suluhu safi za kupikia**, kama vile **mifumo ya biogesi, majiko yaliyoboreshwa, na teknolojia za kupikia zinazotumia sola**, ili kupunguza utegemezi bayomasi asilia na kuboresha afya ya umma.
- Kuhakikisha kwamba mipango ya kikanda kama vile **Misheni ya 300, Ushirikiano Ulioharakishwa wa Bidhaa Jadidifu katika Afrika (Accelerated Partnership for Renewables in Africa, APRA), na Mpango wa Nishati Jadidifu Afrika (Africa Renewable Energy Initiative, AREI) inazingatia jamii, ni shirikishi, na inawanufaisha moja kwa moja watumiaji wa nishati mashinani badala ya kulenga masilahi ya shirika au matajiri**.

## 4. Kuendeleza Haki ya Tabianchi na Suluhu Zinazoongozwa na Afrika

- Kuanzisha **mbinu za kubadilisha ufadhili wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi** ambazo zinakataa **miundo ya ufadhili inayotegemea madeni** na kuwekea kipaumbele **ruzuku, ufadhili kwa masharti nafuu, na mipango ya nishati jadidifu inayoendeshwa na jumuiya**.
- Kuimarisha **muunganisho wa nishati ya bara** kupitia majukwaa kama vile **Umoja wa Afrika (AU), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (REC)** ili kuharakisha maendeleo ya **miundombinu ya nishati safi kimataifa**.

- Kudai kwamba **nchi za Kaskazini mwa Ulimwengu zitimize wajibu wao wa ufadhili wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi**, hasa kwa kuongeza **ufadhili dhidi ya hasara na uharibifu** na kusaidia mabadiliko ya haki ya Afrika bila **masharti ambayo yanadhoofisha mamlaka ya kitaifa na vipaumbele vya maendeleo**.

## 5. Kulinda Watu, Mazingira na Rasilimali katika Mpito wa Nishati

- Kutekeleza **viwango vya lazima vya Idhini ya Bure, ya Awali na kwa Ufahamu (FPIC)** na kuimarisha **haki za umiliki wa ardhi** ili kuzuia unyakuzi wa ardhi na ukiukaji haki za kimazingira katika miradi ya nishati jadidifu.

- Kutekeleza **ulinzi thabiti wa kijamii na kimazingira** katika uchimbaji wa **madini ya mpito** (lithiamu, kobalti, elementi adimu za ardhi), kuhakikisha **mbinu endelevu za uchimbaji madini, manufaa ya jamii, na uongezaji wa thamani wa kindani** kulingana na **Dhamira ya Madini ya Afrika (AMV)**.

- Kusawazisha mpito wa nishati barani Afrika na **malengo ya viwanda vinavyozingatia mazingira** kwa kuwekeza katika **usindikaji na utengenezaji wa ndani wa teknolojia za nishati jadidifu**, kuhakikisha kuwa Afrika **inahifadhi thamani kutoka kwa rasilimali zake badala ya kuendelea kuuza nje malighafi kwa ajili ya viwanda vya nje**.

- Kuanzisha **taratibu za kisheria za uwajibikaji wa shirika** ili kuzuia **madai yanayopotosha ya uzuiaji wa gesijoto na uwekezaji wa unaokandamiza**, kuhakikisha **mifumo ya ugavi wa maadili, uwazi, na umiliki wa Afrika katika mpito wa nishati**.

## Wito wa Kuchukua Hatua

Sisi, mashirika yaliyoweka saini hapa chini, tunazihimiza **serikali za Afrika, mashirika ya kikanda, washirika wa maendeleo, na taasisi za kifedha** kuchukua hatua madhubuti katika kuendeleza **mpito wa nishati jadidifu wenye haki, unaoendeshwa na jamii na wenye mageuzi ya kitasnia**.

Wakati wa uongozi shupavu ni sasa. **Jiunge nasi katika kuifanya Afrika kuwa nguzo ya kimataifa ya nishati jadidifu, haki ya nishati na maendeleo endelevu!**

## Washirika Wanaotusaidia

## Tufuatilie

**Bluesky** - https://bsky.app/profile/wattsupafrica.bsky.social

**Instagram** - https://www.instagram.com/wattsupafrica/